# Maswali

1. Nani walikuwa wakipigana na Waisraeli?
2. Jina la jitu aliitwa nani?
3. Changa moto la Goliathi kwa Waisraeli ilikuwa eti nini?
4. Nani alikuja kwa kambi ya Waisraeli?
5. Mbona Daudi alikasirika?
6. Daudi alisema atafanya nini?
7. Mbona Daudi hakuogopa?
8. Mbona Daudi hakuvaa mavazi ya Sauli?
9. Daudi alienda na nini kupigana na Goliathi?
10. Daudi aliua Goliathi namna gani?

# Majibu

1. Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli.
2. Jitu aliitwa Goliathi.
3. Hebu mtu aje tupigane naye. Nikimua nyinyi mtakuwa watumishi wetu na akiniua sisi tutakuwa watumishi wenu.
4. Daudi alikuja kwa kambi ya Waisraeli.
5. Daudi alikasirika kwa sababu Goliathi alifanyia jeshi la Mungu msaha.
6. Daudi alisema atapigana na Goliathi.
7. Daudi hakuogopa kwa sababu aliamini kwa Mungu. Mungu alikuwa amemwokoa kutoka kwa simba na dubu kwa hivyo angemwokoa kutoka kwa Goliathi.
8. Mavazi ya Sauli ya vita yalikuwa kubwa tena mzito.
9. Daudi alichukua kombeo na mawe 5 kupigia Goliathi.
10. Daudi alipiga Goliathi kwa jiwe kwa kipaji cha kichwa chake, halafu akakata kichwa kwa upanga wake na kukitoa.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1    Mwaka wa 3**

# 27 Daudi na Goliathi

## Marejeo

1 Samweli 17: 2 – 54

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Daudi alikuwa na imani kwa Mungu ya kutosha na alijua atashinda Goliathi.

## Maneno maalum

27.1 Wafilisti + piga Waisraeli + jitu + Goliathi + changa moto + hakuna mtu mjasiri.

27.2 Daudi + kijana mchungaji + Goliathi + Daudi ana hasira + nitapigana + Mungu alisaidia + ua simba na dubu

27.3 Sauli + mavazi yake ya vita + kubwa sana + Daudi + kombeo + mawe 5 + Goliathi ana hasira

27.4 Daudi + ninakuja kwa jina la Bwana Mungu + kombeo na jiwe + piga Goliathi + kipaji cha uso + anguka + Daudi na upanga wa Goliathi + kata kichwa + Mungu alisaidia + Israeli walishinda vita

**27.1** Wafilisti walikuja ili wapigane na Waisraeli. Walipiga kambi kando ya kilima. Jeshi la Waisraeli lilipiga kambi kwa kile kilima upande mwingine. Kulikuwa na bonde katikati yao. Katika jeshi la Wafilisti kulikuwa na jitu kubwa aliyeitwa Goliathi. Alivaa chapeo ya shaba iliyometameta kichwani, mavazi ya vita nzito mwilini mwake mwote na mkuki mkubwa ulikuwa mkononi mwake.

Goliathi alitembea  tembea mbele ya hizo kambi mbili. Alipiga kelele na kuwapa Waisraeli changa moto. "Nawapa nyinyi jeshi la Israeli changa moto. Tuma mtu aje tupigane. Akiniuwa basi, sisi tutakuwa watumishi wenu. Lakini nikishinda hivi vita, nyinyi mtakuwa watumishi wetu."

Kila siku Goliathi alitokea akisema hayo maneno. Lakini hakukuwa na mtu yeyote kwa kambi ya Waisraeli aliyekuwa mjasiri ili apigane na yule jitu.

**27.2** Siku moja Daudi, kijana mchungaji, alikuja kuangalia askari ndugu zake. Alipokuwa anazungumza nao, Goliathi alitokea na kusema maneno yale yale, "Nina mpa changa moto nyinyi jeshi la Israeli…." Daudi aliangalia wanajeshi wote wameogopa na akakasirika sana. Akauliza, "Mfilisti gani huyu asiye na uoga wakutukana jeshi la Mungu aliyehai. Nitaenda nipigane naye."

Mwanzoni wanajeshi walicheka Daudi. Lakini Mfalme Sauli aliposikia, alitumana Daudi aende kwake. Mfalme Sauli aliudhika sana alipoona Daudi kwa vile alikuwa kijana mdogo, mchungaji tu. " Huwezi kupigana na jitu,"aliambia Daudi.

Daudi aliambia Sauli vile Mungu alimsaidia kupiga na kuua simba na dubu wakati alikuwa akichunga kondoo za babake. Aliambia Sauli, "Mungu aliniokoa kutoka kwa simba na dubu. Ataniokoa kutoka kwa jitu, Goliathi."

**27.3** Sauli alipea Daudi mavazi yake ya vita ili avae. Mavazi ya vita ya Sauli yalikuwa kubwa tena mzito sana kwa Daudi, kwa hivyo aliyatoa. Daudi alichukua fimbo na kombeo yake. Alikimbia kwa kijito chini ya bonde. Alichagua mawe tano nyororo kutoka kwa kijito. Halafu akakimbia kwa Goliahi.

Goliathi alipoona Daudi, alikasirika sana kwa sababu aliona Daudi ni mtoto na alikuwa anakuja kupigana naye. Alimpigia kelele akisema, "Mimi ni mbwa ndiyo unakuja kupiga kwa fimbo na mawe? Kuja tu, na nitapea mwili wako kwa wanyama wa kondeni."

**27.4** Daudi aliendea Goliathi kwa ujasiri. Alisema kwa sauti ili wamsikie kule ng'ambo, "Unanikujia kwa upanga, mkuki na ngao, lakini mimi ninakuja katika Jina la Bwana wa Majeshi, Mungu wa jeshi la Israeli. Leo hii Mungu atakuweka mikononi mwangu, ili ulimwengu wote ujue kwamba Israeli kuna Mungu."



Kwa ghadhabu kuu, jitu huyo alikimbia mbele kwa Daudi. Daudi hakuogopa, kwa sababu alijua Mungu ako naye. Haraka haraka Daudi alitia mkono kwa mfuko wa mchungaji na kutoa jiwe aliloliweka kwa kombeo. Kwa uangalifu Daudi alizungusha kombeo juu ya kichwa chake halafu akatupa jiwe kwa nguvu zote. Jiwe lilipiga Goliathi kwa kipaji cha kichwa na akaanguka chini kwa mshindo.

Kulikuwa na kushangilia kwa kambi ya Waisraeli wakati Daudi alikimbia mbele, akachukua upanga wa Goliathi akakata na kutoa kichwa chake. Mungu alisaidia Daudi na Waisraeli kushinda vita.